JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

# MUHTASARI WA KISWAHILI KWA ELIMU YA SEKONDARI

## KIDATO CHA V - VI

2010

TIC 5F24 6327

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

# MUHTASARI WA KISWAHILI KWA ELIMU YA SEKONDARI

## KIDATO CHA V - VI

2010

MAKTABA YA TAASISI YA ELIMU TANZANIA
TAREHE 12/08/2010
S.L.P. 35094 D'SALAAM

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2009

**ISBN: 978-9976-61-272-1**

**Toleo la kwanza: 2009**
**Toleo la Pili: 2010**

Muhtsari huu umetayarishwa na:

**Taasisi ya Elimu Tanzania**
**S.L.P. 35094**
**Dar es salaam**
**TANZANIA**

**Simu: 255 - 22 – 27733005**
**Nukushi: 255 – 22 – 2774420**
**Tovuti: www.tie.go.tz**
**Barua pepe: director.tie@tie.go.tz**

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuigwa, kunakiliwa, kutafsiriwa, kupigwa chapa au kutolewa kwa namna yoyote bila ya idhini ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

# YALIYOMO

Ukurasa

Utangulizi .................... iv
Malengo ya Elimu Tanzania .................... v
Madhumuni ya Elimu ya Sekondari .................... v
Ujuzi wa Jumla wa Somo la Kiswahili .................... vi
Malengo ya Jumla ya Kufundisha Kiswahili katika shule za Sekondari .................... vi
Muundo wa Muhtasari .................... vi
Muda wa Mafunzo .................... viii
Taratibu za upimaji wa somo .................... viii
Kidato cha Tano .................... 1
Kidato cha Sita .................... 34

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Muhtasari wa Kiswahili Kidato cha Tano na cha Sita wa mwaka 2009 utatumika badala ya ule wa mwaka 1997. Muhtasari huu mpya umeandikwa kwa kuzingatia mabadiliko mbalimbali yaliyotokea katika kipindi chote cha utekelezaji wa muhtasari wa mwaka 1997. Mabadiliko yametokea katika nyanja za siasa, uchumi, sayansi, teknolojia, utamaduni na elimu. Mabadiliko yanapotokea huenda sambamba na kukua na kuenea kwa Kiswahili duniani. Kwa mfano, mashirika ya kimataifa kama vile Umoja wa Afrika yameanza kutumia Kiswahili katika shughuli zake. Vyuo vikuu vingi duniani vinafundisha Kiswahili. Vilevile, vyombo vingi vya habari duniani hutumia Kiswahili. Shughuli zote hizi zinaonesha umuhimu wa ufundishaji mzuri wa somo la Kiswahili.

## 1.2 Sababu za Kuboresha Muhtasari na Maboresho Yaliyofanyika

Utafiti uliofanywa mwaka 2008 unaonesha kuwa muhtasari wa mwaka 1997 una upungufu. Upungufu huo umeonekana katika kipengele cha Ujenzi wa ujuzi, malengo na maudhui.

Muhtasari wa mwaka 1997 hauoneshi ujuzi wa jumla wa somo la Kiswahili na ujuzi wa kila kidato. Katika kipengele cha malengo, muhtasari hauoneshi nia ya kumuandaa mwanafunzi kujitegemea, kujiajiri, kujiamini, kuwa mzalendo na kujenga dhana ya kujitegemea katika kujenga stadi za kujifunza katika maisha. Kujenga uzalendo na kujiamini ni muhimu katika jamii. Matokeo ya kujifunza ni bora zaidi pale ambapo mwanafunzi hamtegemei mwalimu tu kwani ujifunzaji endelevu huhitaji stadi za kusoma kwa kujitegemea.

Kutokana na upungufu huo, muhtasari mpya umeonesha ujuzi wa jumla, ujuzi wa kila kidato na maudhui yameboreshwa. Baadhi ya mada mpya zimeingizwa katika muhtasari mpya kutokana na umuhimu wake kwa walengwa ili kukidhi mahitaji ya sasa ya Tanzania na dunia kwa ujumla. Mada hizo ni mada ya tafsiri na ukalimani ambazo zimeingizwa kidato cha tano na kidato cha sita.

Aidha baadhi ya mada na mpangilio wake zimeboreshwa. Katika muhtasari wa mwaka 1997 mada ya historia ya Kiswahili imekuwa Maendeleo ya Kiswahili kwa sababu katika lugha tunajikita zaidi katika maendeleo ya lugha yenye dhana pana zaidi na si historia peke yake. Pia mada ya sarufi imekuwa matumizi ya sarufi ili kueleweka vizuri.
Baadhi ya mada kama vile mada ya fasihi simulizi, ngeli za nomino na utumizi wa lugha zimeondolewa kutoka Kidato cha Sita na kubakizwa Kidato cha tano kwa kuwa zinajitosheleza katika kidato hicho.

Mabadiliko mbalimbali ya kitaaluma, kijamii na kiteknolojia yaliyojiri katika jamii yamesababisha kuingizwa kwa masuala mtambuko kama vile mazingira, UKIMWI, Stadi za maisha, haki za binadamu, usawa wa jinsia, rushwa, teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), dawa za kulevya, ajira ya mtoto, ushauri nasaha na mauaji ya vikongwe na albino. Muhtasari huu pia umejumuisha mbinu shirikishi za kujifunzia na kufundishia zinazojikita kwenye mkabala wa ufundishaji na ujifunzaji unaomjali mwanafunzi na kumjengea ujuzi na utendaji.

## 2.0 Malengo ya Elimu Tanzania

Elimu itolewayo ni ya kurithisha maarifa, stadi na mielekeo bora kutoka vizazi vilivyopita kwa vizazi vya wakati huu na vijavyo. Hivyo yafuatayo ndiyo malengo ya elimu nchini:

- Kujenga na kudumisha stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, ubunifu na mawasiliano.
- Kukuza na kuendeleza mila, desturi na utamaduni wa jamii ya watanzania.
- Kurithisha, kuendeleza na kutumia maarifa, stadi na mielekeo itokanayo na maandishi anuai, sayansi ya jamii, sayansi ya asili, teknolojia na mafunzo ya kazi kuendeleza jamii anamoishi.
- Kukuza na kuendeleza moyo wa kujiamini, kudadisi, kutathmini, kufikiri kiyakinifu na kufanya uamuzi wa busara.
- Kujenga ari ya kujielimisha na utashi wa kuendelea kutafuta maarifa na stadi za kiutendaji.
- Kujenga na kuendeleza heshima kwa Katiba ya Nchi, kuthamini utawala wa sheria na haki za binadamu.
- Kukuza ari ya kuyatambua na kuyahifadhi mazingira.
- Kujenga na kudumisha misingi ya kuthamini umoja, amani na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa.
- Kujenga misingi na ari ya kutambua na kuthamini mchango wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya taifa.

## 3.0 Madhumuni ya Elimu ya Sekondari

Nchini Tanzania elimu ya sekondari ni elimu rasmi inayotolewa kwa vijana waliomaliza elimu ya msingi na kupata sifa za kuingia elimu ya sekondari.

Madhumuni ya ya elimu ya sekondari ni :-

- Kuimarisha na kupanua kina cha mawazo, maarifa, stadi na kanuni zilizofunzwa wanafunzi na kukuzwa katika ngazi ya elimu ya msingi.
- Kuimarisha ukuaji na uthamini wa umoja, utambulisho na maadili ya kitaifa.
- Kuheshimu haki za binadamu, amali za kitamaduni, mila, desturi na wajibu wa kiraia na utayari wa kufanya kazi za aina mbalimbali.
- Kukuza ujuzi wa lugha na kutumia stadi za mawasiliano katika Kiswahili na angalau lugha moja ya kigeni.
- Kutoa fursa ya kupata maarifa, stadi, mielekeo na welewa katika nyanja teule za mafunzo.
- Kuandaa wanafunzi kwa ajili ya elimu ya juu, elimu ya kazi, ufundi na taaluma.
- Kuwajengea wanafunzi uwezo wa kujifunza, kujiamini na teknolojia, maarifa na stadi za kitaaluma na kitaalamu.
- Kuwaandaa wanafunzi kujiunga na dunia ya kazi.

## 4.0 Ujuzi wa Jumla wa Somo la Kiswahili

1) Kuwasiliana kwa Kiswahili kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali.
2) Kuthamini na kutumia Kiswahili kama utamaduni na uzalendo wa mtanzania.
3) Kuandika habari ndefu kwa Kiswahili sanifu.
4) Kusoma na kuelewa habari zenye maarifa mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili.

5) Kutumia lugha ya kisanaa katika mawasiliano.
6) Kuhakiki kazi za fasihi ya Kiswahili.
7) Kujisomea maandiko mbalimbali ya Kiswahili kwa kujitegemea.
8) Kutunga kazi za kitaaluma na kifasihi zinazoweza kuleta kipato.
9) Kutafsiri maandiko mbalimbali kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza na kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili.
10) Kukalimani mazungumzo kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili na kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.

## 5.0 Malengo ya Jumla ya Kufundisha Kiswahili katika Shule za Sekondari

1) Kutumia Kiswahili kwa ufasaha katika fani zote za maisha.
2) Kuhakiki kazi za fasihi ya Kiswahili.
3) Kujenga tabia ya kudadisi masuala ya lugha ya Kiswahili.
4) Kueleza umuhimu wa Kiswahili katika kujenga utamaduni na uzalendo wa Mtanzania.
5) Kubuni kazi mbalimbali za Kiswahili zinazoweza kuleta kipato.
6) Kujenga stadi za kujisomea na kujifunza kwa kujitegemea.
7) Kukuza na kueneza Kiswahili kwa mawasiliano kitaifa na kimataifa.
8) Kutafsiri maandiko mbalimbali kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili na kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.
9) Kukalimani mazungumzo kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili na kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.
10) Kuandika matini mbalimbali za Kiswahili.
11) Kutumia lugha ya Kisanaa katika mawasiliano.
12) Kusikiliza, kusoma na kuelewa matini mbalimbali za Kiswahili.

## 6.0 Muundo wa Muhtasari

Muhtasari huu una sehemu kuu mbili. Sehemu ya Kwanza ni kurasa za awali zinazojumuisha jalada, ukurasa wa jina, ukurasa wa hati miliki, ukurasa wa yaliyomo na utangulizi. Sehemu ya Pili ina majedwali ya ufundishaji yaliyopangwa kulingana na darasa. Kila jedwali la darasa limetanguliwa na ukurasa wenye ujuzi na malengo yanayotarajiwa mwanafunzi kujifunza kwa darasa hilo.

## 6.1 Ufafanuzi wa Vipengele vya Muundo wa Muhtasari wa kila kidato

**Ujuzi**

Ni uwezo na stadi atakazopata mwanafunzi baada ya kujifunza jambo fulani kwa muda maalumu. Ujuzi wa kila kidato umewekwa kabla ya malengo na majedwali ya kila kidato.

**Malengo**

Ni matarajio/mategemeo yanayotazamiwa kufikiwa na mwanafunzi baada ya kujifunza jambo fulani kwa muda maalumu. Malengo ya kila kidato yapo mwanzoni mwa muhtasari kwa kila kidato.

**Majedwali ya ufundishaji na ujifunzaji**

Sehemu kubwa ya muhtasari huu ni majedwali ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kila kidato. Majedwali hayo yana safu zifuatazo:

**Mada/Mada ndogo**: Safu hii inataja kwa kifupi maudhui yatakayoshughulikiwa. Mada kuu imeandikwa kwa herufi kubwa wakati mada ndogo imeoneshwa kwa herufi ndogo. Zingatia kuwa mada ndogo zilizooneshwa ndizo zinazojenga mada kuu.

**Malengo mahususi:** Safu hii inaonesha stadi na mabadiliko ya tabia ambayo mwanafunzi ataweza kuyaonesha baada ya kujifunza mada ndogo. Katika safu hii utendaji wa mwanafunzi ndio unaoonesha kwamba amejifunza.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia:** Hii ni safu inayoonesha vitendo mbalimbali vya mwalimu na wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

**Zana/vifaa:** Hii ni safu inayoonesha orodha ya vitu vinavyomsaidia mwalimu na wanafunzi katika kufikia malengo mahususi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

**Upimaji:** Hii ni safu yenye maswali yanayomwongoza mwalimu kuhusu mambo ya kuzingatia katika kupima kama malengo mahususi yamefikiwa.

**Vipindi:** Hii ni safu inayoonesha idadi ya vipindi vinavyokadiriwa kutosheleza ufundishaji kwa kila mada kuu. Idadi iliyowekwa ni ya kukadiriwa tu. Mwalimu anaweza kurekebisha idadi hiyo kulingana na hali halisi ya wanafunzi wake na mazingira ya ufundishaji kwa ujumla.

**6.2 Ushauri kwa Mwalimu**

Mada za muhtasari zimepangwa kulingana na kidato. Inashauriwa kuwa mada hizi zifundishwe kwa njia ya kuzichanganya na si kwa kufuata mtiririko wa mada uliomo kwenye muhtasari. Kwa mfano, katika wiki moja, mwalimu anaweza kufundisha vipengele vya fasihi kwenye vipindi viwili, sarufi katika kipindi kingine na utungaji katika kipindi kingine. Kwa hiyo ni vema mwalimu aandae azimio la kazi kwa utaratibu huo.

Pia mwalimu anashauriwa kuzingatia yafuatayo:-

1. Pamoja na mbinu za kufundishia zilizoandikwa katika muhtasari huu, mwalimu abuni mbinu nyingine kulingana na uwezo na vionjo vya wanafunzi wake kwa kuzingatia mbinu shirikishi.
2. Atengeneze na kutumia zana na vifaa vya kufundishia kulingana na mahitaji ya wanafunzi wake.
3. Ajielimishe kwa kusoma maandiko mbalimbali yanayochapishwa kila wakati.
4. Awe mfano mzuri wa kuzungumza na kuandika Kiswahili fasaha.

5. Orodha ya vitabu vya kiada na ziada vya kufundishia somo la Kiswahili itakuwa ikitolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kila baada ya muda maalumu.
6. Katika kidato cha tano na cha sita, kila kidato kihakiki vitabu teule vya ushairi, tamthiliya na riwaya.

## 7.0 Muda wa Mafunzo

Somo la Kiswahili ni somo kuu katika Kidato cha Tano na cha Sita. Muda wa mafunzo ni miaka miwili. Somo hili limepangiwa vipindi kumi kwa wiki. Mwalimu anashauriwa atumie vipindi sita kwa ajili ya fasihi na vipindi vinne kwa ajili ya lugha. Kila kipindi ni dakika 40. Siku za masomo ni 194 kwa mwaka. Kila wiki ya masomo ina siku 5. Kwa hiyo wiki za masomo ni takribani 38.8 kwa mwaka. Mitihani ya mihula huchukua wiki mbili kwa mwaka hivyo jumla ya wiki za masomo ni 36. Kwa hiyo jumla ya vipindi kwa kila darasa kwa mwaka ni 360. Vipindi hivyo vimegawanywa katika kila mada kama inavyoonekana kwenye majedwali ya ufundishaji na ujifunzaji. Usambazaji wa idadi ya vipindi iliyokadiriwa umezingatia urefu na ugumu wa mada.

## 8.0 Taratibu za Upimaji wa Somo

Jedwali lifuatalo linaonesha aina za upimaji zitakazotumika kuwapima wanafunzi. Kwa ujumla, kuna aina mbili za upimaji. Kwanza ni upimaji endelezi unaoongozwa na mwalimu katika kupima welewa na utendaji wa mwanafunzi kabla ya, wakati wa, na baada ya kujifunza mada au mada ndogo fulani.Upimaji huu umepewa uzito wa 50% ya alama zote. Pili ni upimaji unaofanywa na Baraza la Mitihani la Taifa na una uzito wa 50% ya alama zote.

Katika upimaji endelezi mwalimu anashauriwa kuwapima wanafunzi kwa kutumia mbinu mbalimbali za upimaji ili kukuza uwezo wa wanafunzi kulimudu somo wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Alama za upimaji endelezi zilizooneshwa katika jedwali hili ni zile tu zitakazounganishwa na alama za upimaji tamati.

| Aina ya upimaji | Mbinu za Upimaji | Fadaa | | | | Uzito (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kidato cha V | | Kidato cha VI | | |
| | | Muhula wa 1 | Muhula wa 2 | Muhula wa 1 | Muhula wa 2 | |
| 1. Upimaji endelezi | 1. Majaribio ya Kuzungumza na kuandika | 2 | 2 | 2 | - | 10 |
| | 2. Kazi mradi | - | - | 1 | - | 5 |
| | 3. Uwasilishaji wa taarifa/hoja kwa mdomo | - | 1 | 1 | - | 5 |
| | 4. Uwasilishaji wa taarifa/hoja kwa kuandika | - | 1 | 1 | - | 5 |
| | 5. Kazi maalumu kwa mwanafunzi mmoja mmoja | 1 | 1 | 1 | - | 5 |
| | 6. Insha | 1 | 1 | - | - | 5 |
| | 7. Mtihani wa muhula | 1 | 1 | 1 | - | 15 |
| Jumla ya alama za upimaji endelezi | | | | | | 50 |
| 2. Mtihani wa mwisho | Mtihani wa Taifa | | | | 1 | 50 |
| JUMLA YA ALAMA | | | | | | 100 |

**Acting Commissioner for Education**
**Ministry of Education and Vocational Training**
**P.O. Box 9121**
**Dar es Salaam**
**Website: www.moe.go.tz**
**Tel: 2110150-2, 2110179**
**Fax: 022113271**

## KIDATO CHA TANO

### Ujuzi wa kidato cha tano

1) Kuwasiliana kwa kuzungumza na kuandika kwa Kiswahili sanifu katika miktadha mbalimbali.
2) Kuandika makala ndefu za kitaaluma na kifasihi kwa Kiswahili sanifu kwa kuzingatia taratibu za uandishi.
3) Kusoma na kuelewa maandiko yenye maarifa mbalimbali kwa kujitegemea.
4) Kufanya tafiti kwenye vipengele vya sarufi na fasihi ya Kiswahili.
5) Kuhakiki kazi za fasihi ya Kiswahili.
6) Kutunga kazi za kitaaluma na kifasihi zinazoweza kuleta kipato.
7) Kuthamini na kutumia Kiswahili kuelezea utamaduni na uzalendo wa mtanzania.
8) Kutafsiri maandiko ya Kiingereza kwenda kwenye Kiswahili na ya Kiswahili kwenda kwenye Kiingereza.
9) Kufanya ukalimani kwa kubadili mazungumzo ya Kiingereza kuwa ya Kiswahili na ya Kiswahili kuwa ya Kiingereza.
10) Kufafanua athari za udhamini wa kazi za kifasihi.
11) Kueleza maendeleo ya Kiswahili katika nyakati mbalimbali.

### Malengo ya kidato cha tano

1) Kufafanua maendeleo ya Kiswahili.
2) Kueleza nadharia ya fasihi na udhamini wa kazi za kifasihi.
3) Kuhakiki kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi.
4) Kujadili maendeleo ya fasihi simulizi na fasihi andishi.
5) Kutunga kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi.
6) Kutumia kanuni za kisarufi kwa usahihi.
7) Kusoma na kuelewa maandiko ya Kiswahili kwa kujitegemea.
8) Kuandika insha, mialiko na barua.
9) Kutambua na kutumia mitindo anuai katika kuzungumza na kuandika.
10) Kutambua na kusahihisha makosa ya kisarufi na kimantiki.
11) Kutafsiri maandiko kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili na kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.
12) Kutumia Kiswahili kuelezea utamaduni na uzalendo wa mtanzania.
13) Kufanya ukalimani kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili na kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.
14) Kutunga kazi za Kiswahili zenye kuleta kipato.
15) Kuchunguza masuala mbalimbali yanayohusu lugha ya Kiswahili.

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| **1.0 MAENDELEO YA KISWAHILI**<br><br>1.1 Asili ya Kiswahili | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili ushahidi wa kihistoria unaothibitisha kuwa Kiswahili ni kibantu. | (i) Kwa kutumia ramani ya Afrika ya mzagao wa wabantu mwalimu awaongoze wanafunzi wakae katika vikundi vidogo vidogo kisha wajadili ushahidi wa kihistoria unaothibitisha kuwa Kiswahili ni kibantu.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kuhusu yaliyowasilishwa. | • Ramani ya Afrika ya mzagao wa wabantu. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili ushahidi wa kihistoria unaothibitisha kuwa Kiswahili ni kibantu? | 12 |
| | b) kufafanua ushahidi wa kiisimu unaothibitisha kuwa Kiswahili ni kibantu. | (i) Kwa kutumia bungua bongo wanafunzi wataje vigezo vya kiisimu vinavyothibitisha kuwa Kiswahili ni kibantu.<br>(ii) Kwa kutumia chati ya miundo mbalimbali ya tungo za kibantu, Kiswahili na lugha zisizo za kibantu, mnyumbuliko wa maneno ya kibantu na Kiswahili na mashina ya vitenzi vya Kiswahili na Kibantu:- wanafunzi wakae kwenye vikundi vidogo vidogo wafafanue ushahidi wa kiisimu unaothibitisha kuwa Kiswahili ni kibantu.<br>(iii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili kwa pamoja yaliyowasilishwa na kufanya maboresho. | • Chati ya miundo mbalimbali ya tungo za kibantu, Kiswahili na lugha zisizo za kibantu<br>• Chati ya mnyumbuliko wa maneno ya kibantu na Kiswahili.<br>• Chati ya mashina ya vitenzi vya Kiswahili na kibantu.<br>• Chati ya sauti za ung'ong'o za lugha ya kiswahili na kibantu | (v) Je, mwanafunzi ameweza kufafanua ushahidi wa kiisimu unaothibitisha kuwa Kiswahili ni kibantu? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | c) kueleza maana na sifa za pijini na kreoli. | (i) Kwa kutumia mchoro wa pembetatu unaoonesha uhusiano wa Pijini na Kreoli wanafunzi wakae katika jozi wajadili maana ya pijini na kreoli.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi.<br>(iii) Kwa njia ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi waeleze sifa za pijini na kreoli. | Mchoro wa pembetatu kuonesha uhusiano wa pijini na kreoli. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza maana na sifa za pijini na kreoli? | |
| | d) kutathmini hoja zinazodai kwamba Kiswahili ni kiarabu, pijini au kreoli. | (i) Katika vikundi vidogo vidogo wanafunzi watathmini hoja zinazodai kwamba kiswahili ni Kiarabu, pijini au kreoli kwa kuzingatia vigezo vya kiisimu na kihistoria.<br>Wanafunzi watumie:-<br>- Chati ya miundo mbalimbali ya tungo za kibantu, Kiswahili na lugha zisizo za kibantu.<br>- Chati ya mnyumbuliko wa maneno ya kibantu na Kiswahili,<br>-Chati ya mashina ya vitenzi vya Kiswahili na kibantu.<br>-Chati ya sauti za ung'ong'o za lugha ya kiswahili na kibantu.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichotathmini.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili kwa pamoja kilichotathminiwa na kufanya maboresho. | • Chati ya miundo mbalimbali ya tungo za kibantu, Kiswahili na lugha zisizo za kibantu<br>• Chati ya mnyumbuliko wa maneno ya kibantu na Kiswahili.<br>• Chati ya mashina ya vitenzi vya Kiswahili na kibantu.<br>• Chati ya sauti za ung'ong'o za lugha ya kiswahili na kibantu | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini hoja zinazodai kwamba Kiswahili ni Kiarabu, pijini au kreoli? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | e) Kufafanua maana na matumizi ya lugha ya kwanza,pili, rasmi na lugha ya Taifa | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome maandiko mbalimbali kuhusu maana na matumizi ya lugha ya kwanza, pili, rasmi na lugha ya Taifa.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Matini mbalimbali kuhusu lugha ya kwanza, pili, rasmi na ya Taifa. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua maana na matumizi ya lugha ya kwanza, pili, rasmi na ya Taifa? | |
| 1.2 Chimbuko la Kiswahili | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kutathmini hoja mbalimbali za chimbuko la Kiswahili. | (i) Kwa kutumia ramani ya Afrika ya mzagao wa wabantu na misafara ya biashara, mwalimu awaongoze wanafunzi wakae katika vikundi vidogo vidogo kisha watathmini hoja ya kuwa chimbuko la Kiswahili ni pwani ya Afrika Mashariki, Kongo au Kameruni.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili kwa pamoja yaliyowasilishwa na kuboresha kazi zao. | • Ramani ya Afrika ya mzagao wa Wabantu.<br>• Ramani ya Afrika ya misafara ya biashara. | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini hoja mbalimbali za chimbuko la Kiswahili? | 12 |
| | b) kujadili sababu za kuibuka kwa lahaja za Kiswahili. | (i) Katika vikundi vidogo vidogo wanafunzi watumie ramani ya Afrika Mashariki ya lahaja mbalimbali za Kiswahili kujadili sababu za kuibuka kwa lahaja za Kiswahili.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili. | • Ramani ya Afrika Mashariki ya lahaja mbalimbali za Kiswahili. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili kuibuka kwa lahaja za Kiswahili? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili kwa pamoja yaliyowasilishwa na kuboresha kazi zao. | | | |
| 1.3 Usanifishaji wa Kiswahili | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili usanifishaji wa Kiswahili wakati wa Mwingereza. | (i) Kwa njia ya majadiliano ya vikundi vidogo vidogo wanafunzi wajadili usanifishaji wa Kiswahili wakati wa Mwingereza.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili kwa pamoja yaliyowasilishwa kisha waboreshe kazi zao.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi watathmini mchoro wa muundo wa kamati ya usanifishaji Kiswahili. | • Mchoro wa muundo wa kamati ya usanifishaji wa Kiswahili. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili usanifishaji wa Kiswahili wakati wa Mwingereza? | 12 |
| | b) kufafanua sababu zilizofanya Kiunguja kiteuliwe kuwa msingi wa kusanifu Kiswahili. | (i) Kwa njia ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi wataje vigezo vinavyotumika kuteua lahaja ya kuisanifisha.<br>(ii) Katika vikundi vyao wanafunzi wajadili sababu zilizofanya kiunguja kiteuliwe kuwa msingi wa kusanifu Kiswahili.<br>(iii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua sababu zilizofanya kiunguja kiwe msingi wa kusanifu Kiswahili? | |
| | c) kujadili kuteuliwa kwa Kiunguja kulivyodumaza | (i) Katika vikundi vyao mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili | | Je, mwanafunzi ameweza kujadili | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | lahaja nyingine za kiswahili. | kuteuliwa kwa kiunguja kulivyodumaza lahaja nyingine.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili na kufanya majadiliano ya pamoja na kuboresha kazi zao. | | kuteuliwa kwa kiunguja kulivyodumaza lahaja nyingine? | |
| 1.4 Changamoto za kuenea kwa Kiswahili katika Afrika Mashariki kabla ya Uhuru | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kutathmini kuenea kwa Kiswahili nchini Tanganyika kabla ya uhuru. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome maandiko mbalimbali yanayoelezea maendeleo ya Kiswahili katika Tanganyika enzi za Mwarabu, Mjerumani na Mwingereza.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi watathmini kuenea kwa Kiswahili nchini Tanganyika kabla ya uhuru.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi.<br>(iv) Kwa kutumia ramani ya Afrika Mashariki ya kuenea kwa Kiswahili mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Ramani ya Afrika Mashariki ya kuenea kwa Kiswahili. | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini kuenea kwa Kiswahili nchini Tanganyika kabla ya uhuru? | 12 |
| | b) kutathmini kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya kabla ya uhuru. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome maandiko mbalimbali yanayoelezea kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya<br>(ii) Wanafunzi watathmini kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya kabla ya uhuru.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi..<br>(iv) Kwa kutumia ramani ya Afrika Mashariki ya kuenea kwa | • Ramani ya Afrika Mashariki ya kuenea kwa Kiswahili. | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya kabla ya uhuru? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiswahili mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kuhusu yaliyowasilishwa kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | | |
| | c) kutathmini kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda kabla ya uhuru. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome na kutathmini maandiko mbalimbali yanayoelezea kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi.<br>(iii) Kwa kutumia ramani ya Afrika Mashariki ya kuenea kwa Kiswahili mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kuhusu yaliyowasilishwa. kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda kabla ya uhuru? | |
| **2.0 FASIHI KWA UJUMLA**<br>2.1 Nadharia ya Fasihi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili mitazamo mbalimbali ya fasili ya fasihi. | (i) Kwa njia ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili mitazamo mbalimbali ya fasili ya fasihi.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili.<br>(iii) Kwa kutumia mchoro wa sanaa na matawi yake mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili kwa pamoja mitazamo mbalimbali ya fasili ya fasihi na kufanya maboresho. | • Mchoro wa sanaa na matawi yake. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili mitazamo mbalimbali ya fasili ya fasihi? | 18 |
| | b) Kufafanua dhima za mtunzi wa kazi za fasihi. | (i) Kwa njia ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi wafafanue dhima za mtunzi wa kazi za fasihi.<br>(ii) Mwalimu atumie njia ya mhadhara mfupi kuhitimisha ufafanuzi wa dhima za mtunzi wa kazi za fasihi. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua dhima za mtunzi wa kazi za fasihi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | c) kufafanua dhima za mhakiki wa kazi za fasihi. | (i) Kwa kutumia bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi wafafanue fasili na dhima za mhakiki wa kazi za fasihi.<br>(ii) Mwalimu atumie njia ya mhadhara mfupi kuhitimisha ufafanuzi wa dhima za mhakiki wa kazi za fasihi. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua dhima za mhakiki wa kazi za fasihi? | |
| | d) kujadili misingi ya uhakiki wa kazi za kifasihi. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome maandiko mbalimbali kuhusu vipengele vya fani na maudhui katika kazi za kifasihi.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wajadili misingi ya uhakiki wa kazi za kifasihi kwa kuzingatia uhusiano wa vipengele vya fani na maudhui.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi.<br>(iv) Mwalimu atumie Chati ya vipengele vya fani na maudhui kuongoza majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Chati ya vipengele vya fani na maudhui. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili misingi ya uhakiki wa kazi za kifasihi? | |
| 2.2 Maendeleo ya Fasihi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza mwanzo wa fasihi. | (i) Wanafunzi wasome maandiko yanayoelezea mwanzo na maendeleo ya fasihi.<br>(ii) Katika vikundi vidogo vidogo wanafunzi wajadili mwanzo wa fasihi.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe walichojadilikwa vikundi.<br>(iv) Mwalimu atoe mhadhara mfupi kuhusu mwanzo wa fasihi. | • Matini na majarida yanayoelezea mwanzo na maendeleo ya fasihi | Je, mwanafunzi ameweza kueleza mwanzo wa fasihi? | 12 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | b) kufafanua kazi za kifasihi katika mifumo mbalimbali. | (i) Kwa njia ya utafiti wanafunzi wasome vitabu na majarida mbalimbali yanayofafanua kazi za fasihi katika mfumo wa ujima, utumwa, ukabaila, ubepari na ujamaa.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichosoma.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kufafanua kazi za fasihi katika mifumo mbalimbali ya maisha ya jamii.<br>(iv) Mwalimu atoe mhadhara mfupi kuhitimisha ufafanuzi wa kazi za fasihi katika mifumo mbalimbali ya maisha ya jamii.<br>(v) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua kazi za fasihi katika mifumo mbalimbali? | |
| 2.3 Uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza fasili ya uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi. | (i) Kwa njia ya maswali na majibu wanafunzi waeleze fasili ya uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wajadili mambo yanayoonesha kuwa mtunzi wa kazi za fasihi ni huru au si huru katika kuandika wa kazi za kifasihi.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi azo. | | Je, mwanafunzi ameweza kueleza fasili ya uhuru wa mwandishi? | 8 |
| | b) kutathmini uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi nchini Tanzania. | (i) Mwalimu awape wanafunzi kazi ya kutafiti watunzi ambao utunzi wao unaonesha kuwa wapo huru na wale ambao hawapo huru. | • Kazi za kifasihi za watunzi mbalimbali. | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi nchiniTanzania? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ii) Katika vikundi vidogo vidogo mwalimu aongoze majadiliano ya kutathmini uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi nchini Tanzania.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe walichojadili.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi watathmini kwa pamoja kuhusu uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi Tanzania. | | | |
| 2.4 Udhamini | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili aina za udhamini wa kazi za kifasihi. | (i) Wanafunzi wasome maandiko yanayoelezea aina za udhamini.<br>(ii) Kwa kutumia majadiliano kwenye vikundi vidogo vidogo wanafunzi wajadili maana na aina za udhamini wa kazi za kifasihi.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe walichojadili.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kuhusu maana na aina za udhamini wa kazi za kifasihi kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Matini na majarida yanayoelezea udhamini wa kazi za kifasihi. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili aina za udhamini wa kazi za kifasihi? | 8 |
| | b) kueleza dhima za udhamini wa kazi za kifasihi. | (i) Kwa njia ya bungua bongo, maswali na majibu na majadiliano, wanafunzi waeleze dhima za udhamini wa kazi za kifasihi.<br>(ii) Mwalimu atoe mhadhara mfupi kueleza dhima za udhamini wa kazi za kifasihi. | | Je, mwanafunzi ameweza kueleza dhima za udhamini wa kazi za kifasihi? | |
| | c) kutathmini athari za udhamini wa kazi za kifasihi. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome na kutathmini maandiko mbalimbali yanayohusu athari za udhamini wa kazi za kifasihi. | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini athari za udhamini wa kazi za kifasihi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi<br>(iii) Kwa njia ya majadiliano ya pamoja mwalimu awaongoze wanafunzi kutathmini athari za udhamini wa kazi za kifasihi. | | | |
| **3.0 MAENDELEO YA FASIHI SIMULIZI**<br>3.1 Uwasilishaji na Uenezaji wa Kazi za Fasihi Simulizi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili uwasilishaji na uenezaji wa kazi za fasihi simulizi. | (i) Kwa kutumia majadiliano ya vikundi wanafunzi wajadili njia mbalimbali za uwasilishaji na uenezaji wa kazi za fasihi simulizi.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboresha kazi zao. | • Chati inayoonesha njia mbalimbali za uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili njia mbalimbali za uwasilishaji na uenezaji wa kazi za fasihi simulizi? | 4 |
| | b) kutathmini athari za sayansi na tekinolojia katika uwasilishaji na uenezaji wa kazi za fasihi simulizi. | (i) Wanafunzi wasikilize na kuangalia kanda zinazoonesha uwasilishaji wa fasihi simulizi.<br>(ii) Kwa njia ya majadiliano wanafunzi wakae katika vikundi vidogo vidogo na kutathmini athari za sayansi na teknolojia katika uwasilishaji na uenezaji wa kazi za Fasihi Simulizi.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe walichojadili.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadilinao ya pamoja kisha wanafunzi waboresha kazi zao. | • Televisheni, vinasa sauti kanda, redio na maandiko ya fasihi simulizi. | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini athari za sayansi na teknolojia katika uwasilishaji na uenezaji wa kazi za Fasihi Simulizi? | |
| 3.2 Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza mbinu mbalimbali | (i) Kwa kutumia njia ya maswali na majibu pamoja na majadiliano ya vikundi, wanafunzi waeleze | | Je, mwanafunzi ameweza kueleza mbinu mbalimbali za | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | za uhifadhi wa fasihi simulizi. | mbinu mbalimbali za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi zake<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi? | |
| | b) kutathmini athari za mbinu mbalimbali za uhifadhi wa fasihi simulizi. | (i) Kwa njia ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi, wajadili ubora na udhaifu wa mbinu mbalimbali za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili kisha mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja.<br>(iii) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini athari za mbinu mbalimbali za uhifadhi wa fasihi simulizi? | |
| 3.3 Kuhakiki Kazi za Fasihi Simulizi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua vipengele muhimu vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi. | (i) Kwa kutumia njia ya masimulizi mwalimu awaongoze wanafunzi wasikilize hadithi na ushairi ulio katika kanda na vinasa sauti kisha wabaini vipengele vya fani na maudhui vilivyojitokeza.<br>(ii) Wanafunzi wakae katika vikundi vidogo vidogo na kujadili kwa kina vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi kama hadithi na ushairi.<br>(iii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili.<br>(iv) Mwalimu atoe mhadhara mfupi kuhusu vipengele muhimu vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi. | • Vinasa sauti, kanda, magazeti na maandiko yenye fasihi simulizi. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua vipengele muhimu vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi? | 16 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (v) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | | | |
| | b) kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi. | (i) Katika vikundi wanafunzi wajadili ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili kisha mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja na kuboresha kazi zao. | Chati inayoonesha vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi. | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi? | |
| | c) Kujadili uhusiano wa vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi. | (i) Wanafunzi wakae katika vikundi vidogovidogo kisha wajadili uhusiano wa vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili kisha mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja na kuboresha kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kujadili uhusiano wa vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi? | |
| | d) Kusoma kazi za fasihi simulizi. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome matini mbalimbali za fasihi simulizi zikiwemo zenye maudhui ya masuala mtambuko kama UKIMWI, ajira ya mtoto, mauaji ya albino, mazingira na usawa wa jinsia.<br>(ii) Kwa njia ya maswali na majibu wanafunzi wachambue vipengele vya fani na maudhui vilivyojitokeza katika matini hizo. | • Matini mbalimbali za kazi za fasihi simulizi. | Je, mwanafunzi ameweza kusoma kwa ufasaha na kuchambua vipengele vya fani na maudhui ya kazi za fasihi simulizi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 3.4 Kutunga Kazi za Fasihi Simulizi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) Kufafanua mbinu za kutunga kazi za fasihi simulizi. | (i) Kwa njia ya majadiliano wanafunzi wakae katika vikundi vidogo vidogo wabaini masuala muhimu ya kuyasimulia kama vile ya masuala mtambuko.<br>(ii) Wanafunzi wapange mawazo yatakayoongoza usimuliaji wa kazi za fasihi simulizi, na kuibua mbinu za kisanaa zitakazojenga kazi za fasihi simulizi watakazozitunga.<br>(iii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili kisha mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja<br>(iv) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Magazeti, majarida na maandiko yanayoelezea mbinu za kutunga kazi za fasihi simulizi. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua mbinu za kutunga kazi za fasihi simulizi? | 14 |
| | b) Kuandika kazi za fasihi simulizi kwa kutumia mbinu za kisanaa. | (i) Wanafunzi wakae katika vikundi vidogo vidogo kisha waandike kazi za fasihi simulizi kama hadithi, semi na mashairi kwa kutumia mbinu za kisanaa.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao kisha mwalimu awaongoze katika majadiliano ya pamoja.<br>(iii) Wanafunzi waboreshe kazi zao.<br>(iv) Mwalimu awape muda wanafunzi wa kutunga michezo ya kuigiza.<br>(v) Wanafunzi waigize darasani kwa vikundi.<br>(vi) Mwalimu awaongoze wanafunzi jinsi ya kuweka michezo ya kuigiza katika maandishi. | | Je, mwanafunzi ameweza kuandika kazi za fasihi simulizi kwa kutumia mbinu za kisanaa? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| **4.0 KUHAKIKI KAZI ZA FASIHI ANDISHI**<br>4.1 Maendeleo ya Fasihi Andishi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili mwelekeo wa kazi za fasihi andishi nchini Tanganyika na zanzibar wakati wa ukoloni. | (i) Kwa njia ya utafiti wanafunzi wasome vitabu mbalimbali vya fasihi vilivyotungwa Tanganyika na Zanzibar wakati wa ukoloni.<br>(ii) Katika vikundi wanafnzi wajadili mwelekeo wa kazi za fasihi andishi nchini Tanganyika na Zanzibar wakati wa ukoloni.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe walichosoma.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja ya muelekeo wa kazi za fasihi andishi nchini Tanganyika na Zanzibar wakati wa ukoloni. | • Vitabu mbalimbali vya fasihi vilivyotungwa Tanganyika na Zanzibar wakati wa ukoloni. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili mwelekeo wa kazi za fasihi andishi nchini Tanganyika na Zanzibar wakati wa ukoloni? | 6 |
| | b) kujadili mwelekeo wa kazi za fasihi andishi nchini Tanzania baada ya uhuru. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome vitabu mbalimbali vya fasihi vilivyotungwa nchini Tanzania baada ya uhuru.<br>(ii) Katika vikundi vidogo vidogo wanafunzi wajadili mwelekeo wa kazi za fasihi andishi nchini Tanzania baada ya uhuru.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe walichosoma.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kuhusu mwelekeo wa kazi za fasihi andishi nchini Tanzania baada ya uhuru. | • Vitabu mbalimbali vya fasihi vilivyotungwa nchini Tanzania baada ya uhuru. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili mwelekeo wa kazi za fasihi andishi nchini Tanzania baada ya uhuru? | |
| 4.2 Kuhakiki Ushairi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili nadharia ya ushairi | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome maandiko yanayoelezea nadharia ya ushairi kulingana na | • Maandiko ya Kiswahili yenye nadharia ya ushairi. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili nadharia ya ushairi | 20 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | kulingana na mtazamo wa kimapokeo na kisasa (mamboleo). | mtazamo wa kimapokeo na wa kisasa.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichosoma.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja na kuboresha walichojadili. | | kulingana na mtazamo wa kimapokeo na wa kisasa? | |
| | b) kujadili vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya ushairi vilivyoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome vitabu teule vya ushairi wakizingatia vipengele vya fani na maudhui.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichosoma.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Matini zinazoelezea uhakiki wa vitabu teule vya ushairi. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya ushairi vilivyoteuliwa? | |
| | c) kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya ushairi vilivyoteuliwa. | (i) Wanafunzi katika vikundi watathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya ushairi vilivyoteuliwa.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walivyotathmini.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi watathmini kwa pamoja ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya ushairi vilivyoteuliwa wakizingatia uhalisia wa maisha ya jamii ya Tanzania. | • Tahakiki za vitabu teule vya ushairi | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya ushairi vilivyoteuliwa? | |
| 4.3 Kuhakiki Riwaya | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya riwaya vilivyoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome vitabu vya riwaya vilivyoteuliwa wakizingatia vipengele vya fani na maudhui.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichojadili. | • Matini zenye uhakiki wa vitabu vya riwaya vilivyoteuliwa | Je, wanafunzi wameweza kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika riwaya zilizoteuliwa? | 20 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wafafanue kwa pamoja walichojadili na kuboresha kazi. | | | |
| | b) kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya riwaya vilivyoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome vitabu vya riwaya vilivyoteuliwa wakizingatia vipengele vya fani na maudhui.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichojadili.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi watathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika kazi za riwaya zilizoteuliwa na kuboresha kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika riwaya zilizoteuliwa? | |
| 4.4 Kuhakiki Tamthiliya | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya tamthiliya vilivyoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome vitabu vya tamthiliya vilivyoteuliwa wakizingatia vipengele vya fani na maudhui..<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichosoma.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafuzni wajadili kwa pamoja kilichowasilishwa na kuboresha kazi zao. | • Matini zenye uhakiki wa Tamthiliya zilizoteuliwa. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya alizosoma? | 20 |
| | b) kutathimini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya tamthiliya vilivyoteuliwa. | (i) Wanafunzi katika vikundi watathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya zilizoteuliwa wakioanisha na uhalisia wa maisha.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walivyotathmini. | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya zilizoteuliwa? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi watathmini kwa pamoja ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya zilizoteuliwa na kuboresha kazi. | | | |
| **5.0 MATUMIZI YA SARUFI**<br>5.1 Matawi ya Sarufi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili maana ya sarufi. | (i) Kwa njia ya maswali na majibu na majadiliano wanafunzi wajadili katika vikundi vyao maana ya sarufi.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe waliyojadili kisha mwalimu aongoze majadiliano kwa pamoja. | • Matini zenye maana na matawi ya safuri. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza maana ya sarufi? | 6 |
| | b) Kufafanua matawi ya sarufi | (i) Wanafunzi wasome vitabu mbalimbali vya sarufi kisha wabainishe matawi ya sarufi.<br>(ii) Kwa njia ya maswali na majibu na majadiliano ya vikundi wanafunzi wafafanue matawi ya sarufi na vipashio vyake.<br>(iii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili kisha mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kwa kutumia mchoro wa matawi ya sarufi na kuboresha kazi zao. | • Mchoro wa matawi ya sarufi<br>• Chati za fonimu, mofimu na tungo mbalimbali. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua matawi ya sarufi? | |
| 5.2 Matumizi ya Mofimu | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya mofimu na mzizi wa neno | (i) Katika vikundi vidogo vidogo wanafunzi wajadili maana ya mofimu na mzizi wa neno na kutoa mifano.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili kisha mwalimu | • Chati ya maneno yenye kuonesha mzizi wa neno na mofimu mbalimbali. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua maana ya mofimu na mzizi wa neno? | 12 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | aongoze majadiliano kwa kutumia chati ya maneno yenye kuonesha mzizi wa neno na mofimu nyingine. | | | |
| | b) kujadili dhima za mofimu | (i) Kwa kutumia majadiliano mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo wajadili dhima za mofimu.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yake kisha mwalimu atumie chati ya maneno yenye kuonesha muainisho wa mofimu kuongoza majadiliano ya pamoja.<br>(iii) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Chati ya maneno yenye muainisho wa mofimu. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili dhima za mofimu? | |
| | c) kuunda maneno kwa kutumia mofimu mbalimbali. | (i) Kwa njia ya majadiliano ya vikundi vidogo vidogo wanafunzi waunde maneno kwa kutumia mofimu mbalimbali.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao kisha mwalimu atumie chati ya mofimu na maneno yaliyoundwa kutokana na mofimu hizo kuongoza majadiliano ya pamoja.<br>(iii) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Chati ya mofimu na maneno yaliyoundwa kutokana na mofimu. | Je, mwanafunzi ameweza kuunda maneno kwa kutumia mofimu mbalimbali? | |
| | d) Kujadili maana ya kiambishi na aina za viambishi. | (i) Kwa njia ya majadiliano wanafunzi wakae katika vikundi vidogo kisha wajadili maana ya viambishi na aina za viambishi.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe walichojadili.<br>(iii) Mwalimu atumie chati ya maneno yanayoonesha viambishi | • Chati ya maneno yaayoonesha viambishi. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza maana ya kiambishi na kujadili aina za viambishi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuongoza majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | | |
| 5.3 Kauli za Kiswahili | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili kauli mbalimbali za kiswahili. | (i) Mwalimu aongoze wanafunzi wasome matini na maandiko mbalimbali kubaini kauli za Kiswahili.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wajadili kauli mbalimbali za lugha ya Kiswahili.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kubaini na kuzifafanua kauli mbalimbali za Kiswahili.<br>(v) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Chati yenye kauli mbalimbali za kiswahili. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili kauli mbalimbali za Kiswahili? | 12 |
| 5.4 Ngeli za Nomino | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza fasili ya ngeli za nomino. | Kwa kutumia bungua bongo mwalimu aongoze wanafunzi kuelewa fasili ya ngeli za nomino. | • Chati ya ngeli za nomino. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza fasili ya ngeli za nomino? | 12 |
| | b) kufafanua ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimapokeo (maumbo) na upatanishi wa kisarufi. | (i) Katika vikundi vidogo vidogo wanafunzi watumie majedwali ya ngeli za nomino kuunda majedwali mengine yanayofanana na hayo.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe majedwali yao.<br>(iii) Mwalimu aongoze wanafunzi kufafanua ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimapokeo na wa upatanishi wa kisarufi kisha, waboreshe kazi zao. | • Jedwali lenye uainishaji wa nomino kwa kufuata mtazamo wa kimapokeo.<br>• Jedwali lenye uainishaji wa nomino kwa kufuata mtazamo wa kisasa. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimapokeo na kisasa? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | c) kujadili ubora na udhaifu wa kila mtazamo. | (i) Katika vikundi wanafunzi watumie majedwali ya ngeli za nomino kujadili ubora na udhaifu wa uainishaji nomino kwa mtazamo wa kimapokeo na wa kisasa.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kuhusu ubora na udhaifu wa uainishaji wa nomino kwa mtazamo wa kisasa na wa kimapokeo.<br>(iv) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Majedwali ya uainishaji wa nomino kwa mtazamo wa kimapokeo na wa kisasa. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili ubora na udhaifu wa kila mtazamo? | |
| 5.5 Matumizi ya ·Orejeshi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua fasili ya o-rejeshi katika sentensi. | (i) Kwa njia ya maswali na majibu wanafunzi wafafanue fasili ya o-rejeshi.<br>(ii) Kwa kutumia chati ya maneno yenye umbo la o-rejeshi mwalimu atoe mhadhara mfupi wa fasili ya o-rejeshi.<br>(iii) Wanafunzi wafanye zoezi la kutunga sentensi zenye o-rejeshi. | • Chati ya maneno mbalimbali yenye umbo la o-rejeshi. | Je, mwanafuzni ameweza kufafanua fasili ya o-rejeshi katika sentensi? | 8 |
| | b) kujadili utokeaji wa umbo la o-rejeshi katika ngeli za nomino. | (i) Katika vikundi wanafunzi wasome jedwali linaloonesha utokeaji wa o-rejeshi katika ngeli za nomino za Kiswahili kisha wajadili utokeaji wa umbo hilo.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichojadili.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Jedwali linaloonesha utokeaji wa umbo la o-rejeshi katika ngeli za nomino | Je, mwanafunzi ameweza kujadili utokeaji wa umbo la o-rejeshi katika ngeli za nomino? | |
| | c) kueleza masharti ya upachikwaji wa o-rejeshi kwenye maneno mbalimbali. | (i) Katika vikundi wanafunzi wabainishe masharti ya upachikwaji wa umbo la o-rejeshi katika maneno mbalimbali ya Kiswahili. | • Chati ya maneno mbalimbali ya Kiswahili yenye umbo la o-rejeshi. | Je, mwanafuzni ameweza kueleza masharti ya upachikwaji wa | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja ya kueleza masharti ya upachikwaji wa umbo la o-rejeshi kwenye maneno mbalimbali ya Kiswahili kwa kutumia chati ya maneno mbalimbali ya Kiswahili yenye umbo la o-rejeshi.<br>(iv) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | | umbo la o-rejeshi kwenye maneno mbalimbali? | |
| | d) kujadili dhima za umbo la o-rejeshi katika tungo za Kiswahili | (i) Katika vikundi wanafunzi wajadili dhima za umbo la o-rejeshi katika tungo.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichojadili.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kuhusu dhima za umbo la o –rejeshi katika tungo za Kiswahili.<br>(iv) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Chati ya maneno mbalimbali ya Kiswahili yenye umbo la o-rejeshi | Je, mwanafunzi ameweza kujadili dhima za umbo la o-rejeshi katika tungo za Kiswahili? | |
| 5.6 Makosa ya Kisarufi na Kimantiki katika Lugha | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili makosa ya kisarufi ya aina mbalimbali katika utumiaji wa lugha na kuyasahihisha. | (i) Wanafunzi wafanye utafiti kwenye vyombo mbalimbali vya habari kuhusu makosa ya kisarufi yanayojitokeza na jinsi ya kuyasahihisha.<br>(ii) Kwa njia ya majadiliano wanafunzi wakae katika vikundi vidogo vidogo kisha wajadili na kubaini makosa ya kisarufi katika sentensi na jinsi ya kuyasahihisha.<br>(iii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao kisha mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja. | • Jedwali la sentensi zenye makosa ya kisarufi. | Je, mwanafunzi ameweza kubaini makosa mbalimbali ya kisarufi na kuyasahihisha? | 8 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kujadili makosa ya kimantiki katika lugha. | (i) Kwa njia ya majadiliano na utafiti wanafunzi katika vikundi vyao wabaini na kusahihisha makosa mbalimbali ya kimantiki katika sentensi, matini za vyombo mbalimbali vya habari.<br>(ii) Baada ya majadiliano na utafiti wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Matini mbalimbali zenye makosa ya kimantiki.<br>• Jedwali la sentensi zenye makosa ya kimantiki. | Je, mwanafunzi ameweza kubaini na kusahihisha makosa ya kimantiki katika lugha? | |
| **6.0 UFAHAMU NA UFUPISHO**<br>6.1 Ufahamu wa kusikiliza na ufupisho | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujibu maswali kutokana na habari aliyoisikiliza. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kusikiliza habari zenye maudhui ya masuala mtambuko zitakazosomwa au kusimuliwa.<br>(ii) Wanafunzi katika jozi wabaini mawazo makuu, maana ya maneno na kutoa hoja binafsi kuhusu walichosikiliza.<br>(iii) Wanafunzi wajibu maswali yatakayoulizwa. | • Majarida, magazeti na matini mbalimbali zenye masuala mtambuko. | Je, mwanafunzi ameweza kujibu maswali kutokana na habari aliyoisikiliza? | 8 |
| | b) Kufupisha kwa mdomo habari aliyoisikiliza. | (i) Wanafunzi wasikilize habari itakayosomwa toka magazetini au matini mbalimbali.<br>(ii) Katika jozi wanafunzi wajadili na kubaini mawazo makuu kutokana na habari waliyoisikiliza.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe mawazo makuu waliyoyabaini yanaweza kuwa ya ugonjwa wa UKIMWI, ufisadi, udhalilishaji wa kijinsia | • Majarida, magazeti na matini mbalimbali zenye masuala mtambuko. | Je, mwanafunzi ameweza kufupisha kwa mdomo habari aliyoisikiliza? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | au mazingira.<br>(iv) Mwalimu aongoze wanafunzi kufupisha kwa mdomo habari waliyoisikiliz | | | |
| 6.2 Ufahamu wa kusoma na ufupisho | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kusoma kwa sauti kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili. | (i) Mwanafunzi mmoja mmoja asome kwa sauti vifungu vya habari vyenye masuala mtambuko.<br>(ii) Mwalimu aongoze wanafunzi wabaini makosa ya kimatamshi yatakayojitokeza na kuyasahihisha. | • Majarida, magazeti na matini mbalimbali zenye masuala ya ukeketaji, mauaji ya albino au ajira ya mtoto. | Je, mwanafunzi ameweza kusoma kwa sauti kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili sanifu? | 8 |
| | b) kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma. | (i) Wanafunzi wasome habari mbalimbali zikiwemo zenye masuala mtambuko kama ugonjwa wa Ukimwi na mauaji ya vikongwe.<br>(ii) Wanafunzi katika jozi wabaini mawazo makuu na maana ya maneno na misemo iliyotumika kwenye habari waliyoisoma.<br>(iii) Mwalimu aongoze wanafunzi wajibu maswali kutokana na habari waliyoisoma. | • Majarida, magazeti na matini mbalimbali zenye masuala mtambuko. | Je, mwanafunzi ameweza kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma? | |
| | c) Kufupisha kwa maandishi habari aliyoisoma. | (i) Wanafunzi wasome matini za majarida, magazeti na matini mbalimbali zenye masuala mtambuko. | • Majarida, magazeti na matini mbalimbali zenye masuala | Je, mwanafunzi ameweza kufupisha kwa maandishi habari aliyoisoma? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ii) Wanafunzi wabaini mawazo makuu kwenye habari.<br>(iii) Mwalimu aongoze wanafunzi wabaini mambo muhimu kwenye ufupisho wa habari.<br>(iv) Wanafunzi wafupishe habari waliyoisoma. | mtambuko. | | |
| **7.0 UTUNGAJI**<br>7.1 Uandishi wa Insha | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha. | (i) Mwalimu atumie bungua bongo, maswali na majibu na majadiliano ya jumla kuwaongoza wanafunzi kutaja mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wafafanue mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha.<br>(iii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yake.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja na kutoa mhadhara mfupi kuhusu mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha.<br>(v) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Matini zenye mitindo mbalimbali ya uandishi wa insha. | • Je, mwanafunzi ameweza kufafanua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha? | 6 |
| | b) Kujadili mitindo mbalimbali ya uandishi wa insha. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome matini zenye mitindo mbali mbali ya uandishi wa insha.<br>(ii) Wanafunzi wajadili mitindo mbalimbali ya uandishi wa insha.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Matini zenye mitindo mbalimbali ya uandishi wa insha. | • Je, mwanafunzi ameweza kujadili mitindo mbalimbali ya uandishi wa insha? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | c) Kuandika insha za hoja, za wasifu na za kisanaa kwa mitindo anuai. | (v) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kuandika insha za hoja, wasifu na kisanaa. Insha hizo zijumuishe maudhui ya elimu ya Ukimwi na usawa wa jinsia. | | Je, mwanafunzi ameweza kuandika insha za hoja, wasifu na kisanaa kwa mitindo anuai? | |
| 7.2 Uandishi wa barua na kadi za mialiko | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili miundo ya uandishi wa barua na kadi za mialiko. | (i) Mwalimu atumie bungua bongo, maswali na majibu kuwaongoza wanafunzi kutaja aina mbalimbali za barua na kazi za mialiko. | • Magazeti, barua na kadi za mialiko. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili miundo ya uandishi wa barua na kadi za mialiko. | 6 |
| | b) kuandika barua na kadi za mialiko ya aina mbalimbali kwa kufuata taratibu za uandishi. | i) Wanafunzi wasome magazeti na kadi za mialiko kisha wachunguze taratibu zake za uandishi.<br>ii) Wanafunzi katika jozi wafanye mazoezi ya kuandika barua na mialiko kwa kuzingatia taratibu zake.<br>iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao<br>iv) Mwalimu awape wanafunzi mazoezi zaidi ya kuandika barua na kadi za mialiko kwa kufuata taratibu za maandishi. | | Je, mwanafuzi ameweza kuandika barua na kadi za mialiko kwa kufuata taratibu za uandishi? | |
| 7.3 Uandishi wa kazi za kifasihi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kutunga kazi fupi mbalimbali za kifasihi kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa kazi hizo. | (i) Mwalimu aongoze wanafunzi wasome matini za kifasihi ili waelewe taratibu za uandishi wa kazi za kifasihi.<br>(ii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kuandika kazi fupi za kifasihi kwa kuzingatia taratibu za uandishi. Kazi hizi zijumuishe maudhui ya Ajira ya Mtoto, Mauaji ya Albino na Jinsia. | • Matini zenye maandishi ya kifasihi | Je, mwanafunzi ameweza kutunga kazi fupi mbalimbali za kifasihi kwa kuzingatia taratibu za uandishi? | 8 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kutunga mashairi, tenzi, ngonjera na tamthiliya mbalimbali. | i) Wanafunzi wafanye kazi mradi na mazoezi ya kuandika ngonjera na tamthiliya.<br>ii) Mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi na kufanya majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kutunga mashairi, tenzi, ngonjera na tamthiliya? | |
| | c) kughani mashairi na tenzi walizoziandika. | (ii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kughani mashairi na tenzi walizoziandika. | | Je, mwanafunzi ameweza kughani mashairi na tenzi? | |
| 7.4 Usimulizi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kupanga mawazo kimantiki katika usimulizi. | (i) Mwalimu atumie maswali na majibu na majadiliano ya jumla kuwaongoza wanafunzi kupanga wa mawazo kimantiki.<br>(ii) Wanafunzi wafanye zoezi la kupanga mawazo kimantiki kwa kusimulia. | • Redio, television, vinasa sauti na kanda za usimulizi wa aina mbalimbali. | Je, mwanafunzi ameweza kutunga kazi fupi mbalimbali za kifasihi kwa kuzingatia upangaji wa mawazo kimantiki? | 6 |
| | b) kutumia mitindo mbalimbali ya uzungumzaji katika usimulizi. | Wanafunzi wafanye mazoezi ya kuzungumza kwa mitindo mbalimbali. | | Je, mwanafunzi ameweza kutumia mitindo mbalimbali katika kusimulia? | |
| | c) kusimulia matukio na hadithi mbalimbali kwa ufasaha. | i) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kusimulia hadithi na matukio mbalimbali kwa vitendo na kwa ufasaha.<br>ii) Mwalimu asahihishe makosa ya kisarufi yanayojitokeza. | | Je, mwanafunzi ameweza kusimulia kwa ufasaha matukio mbalimbali na hadithi? | |
| **8.0 UTUMIZI WA LUGHA**<br>8.1 Rejesta | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kubaini mambo ya kuzingatia anapotumia lugha. | (i) Mwalimu atumie bungua bongo na majadiliano ya jumla kuwaongoza wanafunzi kubaini mambo ya kuzingatia katika kutumia lugha. | • Chati ya rejesta mbalimbali za lugha | Je, mwanafunzi ameweza kubaini mambo ya kuzingatia katika kutumia lugha? | 8 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ii) Kwa kutumia chati ya rejesta mbalimbali za lugha wanafunzi wabaini mambo yaliyozingatiwa katika rejesta hizo.<br>(iii) Kila kikundi kiwaslishe kazi yake.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | | |
| | b) kujadili mitindo mbalimbali ya lugha kulingana na mazingira. | (i) Mwalimu atumie maswali na majibu, majadiliano na uigizaji kuwaongoza wanafunzi kujadili mitindo mbalimbali ya lugha kulingana na miktadha ya lugha.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wajadili mitindo mbalimbali ya lugha.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja.<br>(iv) Wanafnzi waigize mitindo mbalimbali ya lugha. | | Je, mwanafunzi ameweza kujadili mitindo mbalimbali ya lugha kulingana na miktadha? | |
| | c) kufafanua dhima ya rejesta katika lugha. | (i) Katika vikundi wanafunzi wajadili dhima za rejesta.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua dhima za rejesta katika lugha? | |
| | d) kutumia na kuigiza rejesta mbalimbali. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi jinsi ya kutumia na kuigiza rejesta mbalimbali.<br>(ii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kuigiza matumizi ya rejesta. | | Je, mwanafunzi ameweza kutumia rejesta mbalimbali? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 8.2 Misimu | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua maana na aina za misimu. | (i) Kwa njia ya bungoa bongo, maswali na majibu wanafunzi waeleze maana ya msimu na wataje aina za misimu.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wafafanue kwa mifano aina za misimu.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao.<br>(v) Wanafunzi waigize matumizi ya misimu mbalimbali. | • Chati za misimu | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua aina za misimu? | 12 |
| | b) kujadili sifa za misimu. | i) Katika vikundi wanafunzi wajadili sifa za misimu.<br>ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>iii) Mwalimu atumie chati za misimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kujadili sifa za misimu? | |
| | c) kueleza umuhimu wa kutumia misimu katika lugha. | i) Katika vikudni wanafunzi wajadili umuhimu wa kutumia misimu katika lugha.<br>ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao.<br>iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kuhusu umuhimu wa kutumia misimu katika lugha.<br>iv) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kueleza umuhimu wa kutumia misimu katika lugha? | |
| | d) kutathmini changamoto za kutumia misimu katika lugha. | i) Wanafunzi wajadili katika vikundi kuhusu ubora na upungufu wa kutumia misimu katika lugha.<br>ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja. | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini changamoto za kutumia misimu katika lugha? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | e) kufanya utafiti kuhusu misimu mbalimbali katika jamii. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wafanye utafiti kuhusu misimu mbalimbali katika jamiii inayowazunguka.<br>ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja na kisha wanafunzi wasahihishe kazi zao. | | Je mwanafunzi ameweza kufanya utafiti kuhusu misimu mbalimbali katika jamii? | |
| 8.3 Umahiri wa Lugha | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza fasili ya umahiri wa lugha. | Mwalimu atumie majadiliano ya jumla, maswali na majibu kuwaongoza wanafunzi kueleza fasili ya umahiri wa lugha | • Matini zinazoelezea umahiri wa lugha | Je, mwanafunzi ameweza kueleza fasili ya umahiri wa lugha? | 12 |
| | b) kujadili mambo yanayomuwezesha mtu kuwa mahiri wa lugha. | i) Wanafunzi wasome vitabu na matini zinazoeleza umahiri wa lugha.<br>ii) Wanafunzi wawasilishe walichosoma.<br>iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua mambo yanayomwezesha mtu kuwa mahiri wa lugha? | |
| | c) kujadili athari za umahiri wa lugha zaidi ya moja. | v) Katika vikundi wanafunzi wajadili athari za umahiri wa lugha zaidi ya moja.<br>vi) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>vii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja na kutoa mhadhara mfupi kuhusu athari za umahiri wa lugha zaidi ya moja. | | Je, mwanafunzi ameweza kujadili athari za umahiri wa lugha zaidi ya moja? | |
| | d) kufafanua mambo yanayopoteza umahiri wa lugha. | i) Katika vikundi wanafunzi wafafanue mambo yanayopoteza umahiri wa lugha. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua mambo yanayopoteza umahiri wa lugha? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>iii) Mwalimu atumie majadiliano ya pamoja kufafanua mambo yanayopoteza umahiri wa lugha. | | | |
| 8.4 Utata katika matumizi ya lugha | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kubaini tungo zenye utata na jinsi ya kuondoa utata. | (i) Kwa kutumia chati yenye tungo zenye utata wanafunzi wabaini utata katika tungo hizo.<br>(ii) Wanafunzi katika vikudni wajadili jinsi ya kuondoa utata kazika tungo.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Chati yenye tungo zenye utata | Je, mwanafunzi ameweza kubaini tungo zenye utata na jinsi ya kuondoa utata katika tungo? | 8 |
| | b) kufafanua chanzo cha utata katika mawasiliano. | (i) Wanafunzi wajadili kwa vikundi chanzo cha utata katika mawasiliano.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja na kisha wanafunzi waboresha kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua chanzo cha utata? | |
| | c) kujadili jinsi ya kuondoa utata katika mawasiliano. | (i) Katika vikundi wanafunzi wajadili jinsi ya kuondoa utata katika mawasiliano.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kwa kutumia chati | • Chati ya tungo zenye utata na chati ya tungo zilizoondolewa utata. | Je, mwanafunzi ameweza kujadili jinsi ya kuondoa utata katika mawasiliano? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ya tungo zenye utata na chati ya tungo zilizoondolewa utata kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | | |
| **9.0 TAFSIRI NA UKALIMANI**<br>9.1 Tafsiri | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya tafsiri. | (i) Wanafunzi wasome vitabu na matini zenye tafsiri mbalimbali kisha waeleze maana ya tafsiri<br>(ii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kupata maana sahihi ya tafsiri. | • Matini zilizotafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza na kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili | Je, mwanafunzi ameweza kueleza maana ya tafsiri? | 12 |
| | b) kufafanua mambo ya kuzingatia wakati wa kutafsiri. | (i) Kwa njia ya majadiliano ya vikundi wanafunzi wafafanue mambo ya kuzingatia wakati wa kutafsiri.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua mambo ya kuzingatia wakati wa kutafsiri? | |
| | c) kutafsiri matini fupi mbalimbali za Kiswahili kwenda lugha ya Kingereza na za lugha ya Kingereza kwenda Kiswahili. | (i) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kutafsiri matini fupi za Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili kwa vikundi.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao.<br>(iii) Mwalimu atoe maboresho kwa kila kikundi.<br>(iv) Mwanafunzi mmojammoja atafsiri matini fupi mbalimbali za | | Je, mwanafunzi ameweza kutafsiri matini fupi kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiswahili kwenda lugha ya Kingereza na za lugha ya Kingereza kwenda Kiswahili.<br>(v) Mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi. | | | |
| 9.2 Ukalimani | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ukalimani | (i) Wanafunzi wasome vitabu na matini zinazohusu ukalimani.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wajadili maana ya ukalimani na kuwasilisha kazi zao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja k isha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Makala au matini zinazohusu ukalimani | Je, mwanafnzi ameweza kueleza maana ya ukalimani? | 12 |
| | b) kujadili mambo ya kuzingatia wakati wa ukalimani. | (i) Wanafunzi wajadili katika vikundi kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa kukalimani.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja na kisha wanafunzi waboresha kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kujadili mambo ya kuzingatia wakati wa kukalimani? | |
| | c) Kukalimani mazungumzo mafupi ya Kiswahili kwenda Kiingereza na kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. | Wanafunzi wafanye mazoezi ya kukalimani mazungumzo ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza na kwenda Kiswahili. | | Je, mwanafunzi ameweza kukalimani mazungumzo mafupi ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili? | |

## KIDATO CHA SITA

**Ujuzi wa kidato cha sita**

Mwanafunzi akimaliza kidato cha sita aoneshe uwezo wa:

1) Kueleza maendeleo ya Kiswahili.
2) Kusoma na kuelewa habari ndefu zilizoandikwa kwa Kiswahili.
3) Kuandika habari kwa kuzingatia taratibu za uandishi.
4) Kuhakiki kazi za fasihi andishi.
5) Kutunga na kuigiza kazi za fasihi andishi.
6) Kutumia mitindo mbalimbali ya uzungumzaji na uandishi.
7) Kutumia kanuni za kisarufi na kimantiki kwa usahihi.
8) Kutafsiri maandiko yaliyo katika lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza na kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili.
9) Kufanya ukalimani kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili na kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.
10) Kubuni kazi mbalimbali za kiswahili zinazoweza kuleta kipato.

**Malengo ya kidato cha sita**

Mwishoni mwa kidato cha sita mwanafunzi aweze:

1) Kueleza maendeleo ya Kiswahili.
2) Kuhakiki kazi za fasihi simulizi.
3) Kutunga na kuigiza kazi za fasihi simulizi.
4) Kutumia kanuni za kisarufi kwa usahihi.
5) Kusoma na kuelewa maandiko ya Kiswahili.
6) Kuandika insha, risala, hotuba, matangazo na barua.
7) Kubainisha na kutumia mitindo mbalimbali ya uzungumzaji na uandishi.
8) Kubainisha na kusahihisha makosa ya kisarufi na kimantiki.
9) Kutafsiri maandiko kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili na kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.
10) Kufanya ukalimani kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili na kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.
11) Kutunga kazi mbalimbali za Kiswahili zenye kuleta kipato.

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| **1. 0 MAENDELEO YA KISWAHILI**<br><br>1.1 Ukuaji na Uenezaji wa Kiswahili nchini Tanzania baada ya Uhuru | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Tanzania kukuza Kiswahili baada ya Uhuru. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome maandiko mbalimbali yanayoeleza hatua zilizochukuliwa na serikali ya Tanzania na asasi zisizo za kiserikali kukuza Kiswahili baada ya uhuru.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wawasilishe walichosoma na kujadiliana kwa pamoja.<br>(iii) Mwalimu atumie chati ya asasi za kukuza Kiswahili kukazia ujuzi wa wanafunzi kuhusu hatua zilizochukuliwa na serikali kukuza Kiswahili baada ya uhuru.<br>(iv) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Chati inayoonesha asasi anuai za kukuza na kueneza Kiswahili Tanzania baada ya uhuru. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza hatua zilizochukuliwa na serikali kukuza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru? | 22 |
| | b) kufafanua madhumuni ya vyombo na Taasisi zilizokuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa maswali na majibu kutaja madhumuni ya vyombo na Taasisi zilizokuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.<br>(ii) Katika vikundi vidogo vidogo wanafunzi wafafanue madhumuni ya vyombo na Taasisi zinazokuza na kueneza | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua madhumuni ya vyombo na Taasisi zilizokuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kiswahili nchini Tanzania<br>(iii) Mwalimu atumie chati ya asasi za kukuza na kueneza Kiswahili kusisitiza madhumuni ya asasi hizo. | | | |
| | c) kujadili mafanikio na changamoto za vyombo na taasisi hizo katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.. | (i) Wanafunzi wajadili katika vikundi kuhusu mafanikio na changamoto za vyombo na taasisi za kukuza na kueneza Kiswahili Tanzania.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kujadili mafanikio na changamoto za vyombo vya kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru? | |
| 1.2 Ukuaji na Ueneaji wa Kiswahili nchini Kenya na Uganda baada ya uhuru | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza hatua zilizochukuliwa na serikali ya Kenya na Uganda kukuza na kueneza Kiswahili katika nchi hizo baada ya uhuru. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome kwa kujitegemea maandiko anuai yanayoelezea ukuaji na ueneaji wa Kiswahili nchini Kenya na Uganda baada ya uhuru.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe mambo waliyosoma na kuyajadili<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi wafanye maboresho. | • Matini mbalimbali zinazoelezea ukuaji na uenezaji wa Kiswahili nchini Kenya na Uganda baada ya Uhuru. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza hatua zilizochukuliwa na serikali ya kenya na Uganda kukuza na kueneza Kiswahili katika nchi hizo baada ya uhuru? | 18 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | b) kufafanua madhumuni ya vyombo vya serikali na visivyo vya serikali katika kukuza Kiswahili nchini Kenya na Uganda. | (i) Katika vikundi wanafunzi wafanye kazi mradi ya kutafiti madhumuni, mafanikio na changamoto za asasi za serikali na zisizo za serikali katika kukuza Kiswahili nchini Kenya na Uganda.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao.<br>(iii)Mwalimu awaongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua madhumuni ya vyombo vya serikali na visivyo vya serikali katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya na Uganda baada ya uhuru? | |
| | c) kujadili mafanikio na changamoto za asasi za serikali na zisizo za serikali katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya na Uganda baada ya uhuru. | (i) Kwa njia ya majadiliano ya vikundi wanafunzi wajadili mafanikio na changamoto za asasi za serikali na zisizo za serikali katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya na Uganda baada ya uhuru.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao | | Je, mwanafunzi ameweza kujadili mafanikio na changamoto za asasi za serikali na zisizo za serikali katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya na Uganda baada ya uhuru? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.3 Ukuaji na ueneaji wa Kiswahili duniani | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza jinsi Kiswahili kilivyoenea na kukua katika nchi mbalimbali duniani. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome maandiko anuai pamoja na tovuti kuhusu ukuaji na uenezaji wa Kiswahili duniani kote.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi waeleze jinsi Kiswahili kilivyoenea na kukua katika nchi mbalimbali duniani.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iv) Mwalimu atoe mhadhara mfupi kueleza jinsi Kiswahili kilivyokua na kuenea duniani | • Ramani ya dunia inayoonesha nchi zenye vituo vya redio na vyuo vikuu vinavyotumia na kufundisha Kiswahili. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza ukuaji na ueneaji wa Kiswahili duniani? | 10 |
| | b) kujadili mafanikio na changamoto za kukua na kuenea kwa Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani. | (i) Katika vikundi vidogo vidogo wanafunzi wasome maandiko mbalimbali na kujadili mafanikio na changamoto za kukua na kuenea kwa kiswahili katika nchi mbalimbali duniani<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichosoma kwa vikundi.<br>(iii) Mwalimu atumie ramani ya dunia kuonesha vituo na vyuo vikuu vinavyotumia Kiswahili kuhitimisha majadiliano.<br>(iv) Wanafunzi waboreshe kazi zao | | Je, mwanafunzi ameweza kujadili mafanikio na changamoto za kukua na kuenea kwa kiswahili katika nchi mbalimbali duniani? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| **2.0 UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI**<br>2.1 Uhakiki wa Ushairi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili vipengele vya fani na maudhui ya vitabu vya ushairi vilivyoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa vikundi wasome matini na vitabu teule vya ushairi wakizingatia vipengele vya fani na maudhui.<br>(ii) Wanafunzi wajadili vipengele vya fani na maudhui ya vitabu vya ushairi vilivyoteuliwa.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe walichojadili<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao | • Matini mbalimbali zinazoelezea vipengele vya fani na maudhui katika ushairi<br>• Tahakiki mbalimbali za ushairi | Je, mwanafunzi ameweza kujadili vipengele vya fani na maudhui ya vitabu vya ushairi vilivyoteuliwa? | 30 |
| | b) kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika vitabu vya ushairi vilivyoteuliwa. | (i) Wanafunzi katika vikundi wajadili ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui ya vitabu vya ushauiri walivyosoma.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichojadili.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui vya vitabu teule vya ushairi? | |
| 2.2 Uhakiki wa Riwaya | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili vipengele vya fani na maudhui ya vitabu vya riwaya vilivyoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome na kujadili vitabu teule vya riwaya wakizingatia vipengele vya fani na maudhui.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe | • Matini mbalimbali zinazoelezea vipengele vya fani na maudhui katika riwaya<br>• Tahakiki | Je, mwanafunzi ameweza kujadili vipengele vya fani na maudhui ya vitabu vya riwaya vilivyoteuliwa? | 30 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | walichojadili.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja na kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | mbalimbali za riwaya | | |
| | b) kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui ya vitabu vya riwaya vilivyoteuliwa. | (i) Katika vikundi wanafunzi wajadili ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui ya vitabu vya riwaya walivyosoma.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe walichojadili kwa vikundi.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini vipengele vya fani na maudhui katika riwaya zilizoteuliwa? | |
| 2.3 Uhakiki wa Tamthiliya | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili vipengele vya fani na maudhui ya vitabu vya tamthiliya vilivyoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome na kujadili vitabu teule vya tamthiliya wakizingatia vipengele vya fani na maudhui.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Matini mbalimbali zinazoelezea uhakiki wa tamthiliya | Je, mwanafunzi ameweza kujadili vipengele vya fani na maudhui vya vitabu vya tamthiliya vilivyoteuliwa? | 30 |
| | (b) kutathmini ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na maudhui katika | i) Wanafunzi wajadili katika vikundi ubora na udhaifu wa vipengele vya fani na | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini vipengele vya fani na | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | vitabu vya tamthiliya vilivyoteuliwa. | maudhui ya vitabu vya tamthiliya teule.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kwa vikundi walichojadili.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | maudhui katika vitabu vya tamthiliya vilivyoteuliwa? | |
| 2.4 Usanifu wa Maandishi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kusanifu maandishi ya kifasihi. | (i) Katika vikundi wanafunzi wasome matini mbalimbali za kifasihi na kujadili mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kusanifu maandishi ya kifasihi<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe waliyoyajadili kwa vikundi.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Matini mbalimbali za kifasihi | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua mambo ya kuzingatia wakati wa kusanifu maandishi ya kifasihi? | 24 |
| | b) kutathmini ubora na udhaifu wa maandishi ya kifasihi. | (i) Mwanafunzi mmoja mmoja asome maandishi ya kifasihi.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wajadili ubora na udhaifu wa maandishi mbalimbali ya kifasihi.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao za vikundi kisha wajadili kwa pamoja<br>(iv) Mwalimu atoe mhadhara mfupi kuhusu ubora na udhaifu wa maandishi ya kifasihi. | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini maandishi ya kifasihi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | c) kujibu maswali mbalimbali kutokana na maandishi au habari aliyoisoma. | (i) Mwalimu awape wanafunzi habari ya kusoma<br>(ii) Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kutokana na habari waliyoisoma.Mwanafunzi mmoja mmoja ajibu maswali kutokana na habari aliyoisoma. | | Je, mwanafunzi ameweza kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma? | |
| **3.0 MATUMIZI YA SARUFI**<br>3.1 Ufafanuzi wa Tungo | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua aina za tungo. | (i) Mwalimu atumie njia ya maswali na majibu na bungua bongo kuwaongoza wanafunzi wataje aina za tungo.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wafafanue aina za tungo.<br>(iii) Kila kikundi kiwasilishe kazi zake.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Mchoro wa tungo na aina zake | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua aina za tungo? | 24 |
| | b) kujadili vipashio vya kirai, kishazi na sentensi. | (i) Wanafunzi wajadiliane katika vikundi kuhusu vipashio vya kirai, kishazi na sentensi.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Chati ya virai, vishazi na sentensi | Je, mwanafunzi ameweza kujadili vipashio vya kirai, kishazi na sentensi? | |
| | (c) kujadili dhima za kirai, kishazi na sentensi. | (i) Katika vikundi wanafunzi wajadili dhima za kirai, kishazi na sentensi. | | Je, mwanafunzi ameweza kujadili dhima za kirai, kishazi na sentensi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ii) Wanafunzi wawasilishe kazi ao kwa vikundi.<br>(ii) zMwalimu atoe mhadhara mfupi kuhitimisha yaliyojadiliwa.<br>(iii) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | | | |
| 3.2 Uchanganuzi wa Sentensi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua hatua muhimu katika uchanganuzi wa sentensi. | (i) Katika vikundi wanafunzi wasome matini mbalimbali za uchanganuzi wa sentensi kisha wafafanue hatua za uchanganuzi wa sentensi.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao.<br>(iii) Kwa kutumia chati ya uchanganuzi wa sentensi mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kufafanua hatua za uchanganuzi wa sentensi.<br>(iv) Wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Chati za uchanganuzi wa sentensi | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua hatua za uchanganuzi wa sentensi? | 20 |
| | b) kuchanganua sentensi kwa njia ya matawi, jedwali/visanduku, maelezo na mishale. | (i) Wanafunzi katika vikundi wafanye mazoezi ya kuchanganua sentensi mbalimbali kwa njia za matawi, jedwali/visanduku, maelezo, mishale.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | | Je, mwanafunzi ameweza kuchanganua sentensi kwa njia za matawi, jedwali/visanduku, maelezo na mishale? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 3.3 Uundaji wa Maneno | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua sababu za uundaji wa maneno ya Kiswahili. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome vitabu na matini zenye kuelezea uundaji wa maneno ya Kiswahili kisha wabaini sababu za uundaji wa maneno hayo.<br>(ii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja. | • Chati za uundaji wa maneno ya Kiswahili | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua sababu za uundaji wa maneno ya Kiswahili? | 28 |
| | b) kujadili njia mbalimbali za uundaji wa maneno. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wasome maandiko mbalimali yanayoelezea njia mbalimbali za uundaji wa maneno.<br>(ii) Wanafunzi wajadili njia mbalimbali za uundaji wa maneno.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi.<br>(iv) Kwa kutumia chati ya uundaji wa maneno mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Chati inayoonesha njia mbalimbali za uundaji wa maneno | Je, mwanafunzi ameweza kujadili njia mbalimbali za uundaji wa maneno? | |
| | c) kuunda maneno mapya ya Kiswahili. | (i) Katika vikundi wanafunzi wafanye mazoezi ya kuunda maneno mapya ya Kiswahili.<br>(ii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao | | Je, mwanafunzi ameweza kuunda maneno ya Kiswahili? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao | | | |
| 4 KUTUNGA HABARI<br>4.1 Kuandika Habari | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa risala, hotuba, wasifu binafsi na matangazo. | (i) Mwalimu atumie bungua bongo na majadiliano kuwaongoza wanafunzi kutaja mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa risala, hotuba, wasifu binafsi na matangazo.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wafafanue mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa risala, hotuba, wasifu binafsi na matangazo.<br>(iii) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa vikundi<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao. | • Magazeti, chati za matangazo na matini zenye risala, hotuba, wasifu binafsi na matangazo | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa risala, hotuba, wasifu binafsi na matangazo? | 26 |
| | b) kuandika risala, hotuba, wasifu binafsi na matangazo. | i) Katika vikundi wanafunzi wafanye mazoezi ya kuandika risala, hotuba, matangazo na wasifu binafsi kuhusu mazingira, Mmomonyoko wa maadili, maendeleo ya sayansi na tekinolojia na UKIMWI.<br>ii) Kila kikundi kiwasilishe walichoandika na kufanya | | Je, mwanafunzi ameweza kuandika risala, hotuba, wasifu binafsi na matangazo? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | majadiliano ya pamoja.<br>iii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja. | | | |
| 4.2 Usimulizi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kupanga mawazo kimantiki katika kutoa taarifa kwa kuzungunza. | (i) Mwalimu atumie bungua bongo na majadiliano ya jumla kuwaongoza wanafunzi kupanga mawazo kimantiki katika kutoa taarifa kwa kuzungumza.<br>(ii) Mwanafunzi mmoja mmoja atoe taarifa kwa kuzungumza kuhusu mambo muhimu yanayojitokeza katika jamii kama kilimo, maendeleo ya viwanda, ufisadi, mazingira na madawa ya kulevya<br>(iii) Mwalimu aongoze wanafunzi wajadili kwa pamoja jinsi walivyowasilisha na kurekebisha makosa yao. | • Vinasa sauti na kanda mbalimbali zilizorekodi sanaa ya uzungumzaji hadharani | Je, mwanafunzi ameweza kupanga mawazo kimantiki katika kutoa taarifa kwa kuzungumza? | 28 |
| | b) kutumia sanaa ya uzungumzaji hadharani. | (i) Wanafunzi wasikilize na kuangalia kanda za video zilizorekodi usimulizi wa kisanaa hadharani.<br>(ii) Mwalimu aongoze majadiliano ya jumla kuhusu mambo muhimu katika sanaa ya uzungumzaji hadharani. | | Je, mwanafunzi ameweza kutumia sanaa ya uzungumzaji hadharani? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kutumia sanaa ya kuzungumza hadharani. Mada za kuzungumza zihusishe pia masuala mtambuko. | | | |
| 4.3 Kutunga kazi za Kifasihi | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kutunga kazi ndefu za kifasihi kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa kazi za kifasihi. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome maandiko mbali mbali yanayoelezea taratibu za uandishi wa kazi za kifasihi<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wajadili mambo ya kuzingatia katika kutunga kazi za kifasihi.<br>(iii) Kila kikundi kiwasilishe kazi yao.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao.<br>(v) Kwa njia ya kazi mradi wanafunzi watunge na kuandika kazi ndefu za kifasihi.<br>(vi) Wanafunzi wawasilishe kazi zao kwa mwalimu. | • Matini za kifasihi na magazeti yenye maandiko ya kifasihi. | Je, mwanafunzi ameweza kutunga kazi ndefu za kifasihi kwa kuzingatia taratibu za uandishi? | 24 |
| | b) kutathmini kazi ndefu za kifasihi kwa kuzingatia taratibu za uandishi. | (i) Baada ya kuwasilisha kazi mradi za kifasihi walizotunga wanafunzi; mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kutathmini kazi hizo. | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini kazi ndefu za kifasihi kwa kuzingatia taratibu za uandishi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ii) Wanafunzi warekebishe kazi zao. | | | |
| 5 KUTAFSIRI NA KUKALIMANI<br>5.1 Kutafsiri | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kutafsiri matini ndefu mbalimbali za Kiswahili kutoka lugha ya Kingereza na kwenda lugha ya Kiswahili na Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza. | (i) Mwalimu atumie mbinu ya mazoezi na kazi mradi kuwaongoza wanafunzi watafsiri matini za Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wafanye mazoezi ya kutafsiri matini za Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili.<br>(iii) Kila kikundi kiwasilishe kazi zake.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kisha wanafunzi waboreshe kazi zao.<br>(v) Mwanafunzi mmoja mmoja afanye mazoezi ya kutafsiri matini za Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili.<br>(vi) Mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi | • Matini zenye tafsiri za Kiswahili kwenda Kingereza na Kingereza kwenda Kiswahili. | Je, mwanafunzi ameweza kutafsiri matini ndefu mbalimbali za Kiswahili kwenda lugha ya Kingereza na Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili? | 24 |
| | b) kutathmini kazi za tafsiri walizozifanya wanafunzi kwa njia ya kazi mradi kutoka Kiswahili kwenda | (i) Wanafunzi wawasilishe kazi mradi za tafsiri walizofanya.<br>(ii) Mwalimu aongoze | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini kazi za tafsiri walizofanya kutoka | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili. | wanafunzi watathmini kwa pamoja na kuboresha kazi zao. | | Kiswahili kwenda Kiingereza na kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili? | |
| 5.2 Kukalimani | Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanafunzi aweze:<br>a) kukalimani mazungumzo marefu ya Kiswahili kwenda Kingereza na Kingereza kwenda Kiswahili | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wafanye mazoezi ya kukalimani mazungumzo marefu ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili.<br>(ii) Katika vikundi wanafunzi wafanye mazoezi ya kukalimani mazungumzo marefu ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili.<br>(iii) Mwanafunzi mmoja mmoja afanye mazoezi ya kukalimani mazungumzo marefu ya Kiswahili kwenda Kingereza na Kingereza kwenda Kiswahili.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja. | | Je, mwanafunzi ameweza kukalimani mazungumzo marefu ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili? | 24 |
| | b) kutathmini ukalimani uliofanywa toka Kiswahili kwenda Kingereza na Kingereza kwenda Kiswahili. | (i) Wanafunzi katika jozi wafanye ukalimani na wenzao watathmini. mazungumzo yao.<br>(ii) Mwalimu aongoze majadiliano ya pamoja kutathmini jinsi | | Je, mwanafunzi ameweza kutathmini ukalimani wa mazungumzo marefu ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | IDADI YA VIPINDI ILIYOKADIRIWA |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | walivyokalimani mazungumzo toka Kiswahili kwenda Kingereza na Kingereza kwenda Kiswahili<br>(iii) Wanafunzi wafanye mazoezi zaidi na kusahihisha makosa yao. | | Kiswahili? | |

TAASISI YA ELIMU TANZANIA

ELIMU NI KAZI

Printed by: Business Printers Ltd, 16 Lugoda Street Gerezani Industrial Area.
P.O. Box 78495, Dar es salaam, Tel: (22) 2134060/2134062